

TUZO YA MWANDISHI BORA WA HABARI ZA KITAKWIMU MWAKA 2019

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa mujibu wa Sheria No. 9 ya Mwaka 2015 pamoja na Marekebisho yake (ya mwaka 2018 na 2019) ndio yenyewe mamlaka ya kisheria ya kuratibu na kusimamia uzalishaji na usambazaji takwimu nchini.

Katika kutekeleza majukumu yake hayo NBS inashirikiana na wadau mbali mbali wa ndani na nje. Vyombo vya habari ni moja kati ya wadau wakubwa wa NBS katika kufanikisha utekelezaji majukumu yake hayo ya kila siku ya kuratibu na kusimamia uzalishaji na usambazaji wa takwimu nchini.

Katika kuhakikisha kuwa vyombo vya habari vinatekeleza wajibu wake wa kuelimisha na kuhabarisha jamii kuhusu masuala ya kitakwimu, NBS imekuwa ikitoa mafunzo ya mara kwa mara kuimarisha uwezo wa vyombo hivyo kutangaza na kuandika habari za kitakwimu kwa weledi na ufasaha ili viweze kuwasilisha vyema ujumbe sahihi wa kitakwimu kwa walengwa.

Katika kuhamasisha uandishi bora wa kitakwimu, NBS imeamua kuanzisha tuzo kwa vyombo vya habari vinavyoandika habari za kitakwimu na mwandishi bora wa habari za kitakwimu kuanzia mwaka 2019. Tuzo za mwandishi bora zitakuwa zikitolewa siku ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Takwimu Afrika ambayo hufanyika mwezi Novemba kila mwaka. Mwaka huu, kwa Tanzania, Maadhimisho hayo yatafikia kilele tarehe 28 Novemba, 2019 na yatafanyika katika ukumbi wa mikutano wa Kituo Cha Mikutano Cha Kimataifa cha Mwalimu Nyerere kilichopo Mtaa wa Shaaban Robert jijini Dar es salaam.

NBS imeanzisha tuzo hii ikiwa ni ishara ya kutambua na kuthamini uandishi wa habari za kitakwimu ambao umeandika kiuchambuzi na kiufasaha takwimu mbalimbali zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuwawezesha wananchi kuelewa ujumbe sahihi uliobeba takwimu husika. Aidha, tunatarajia kuwa tuzo hii itawahamasisha na kuwashajiisha waandishi wa habari kutumia takwimu kuchambua, kuhoji na kuchunguza masuala yanayoisibu jamii ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa takwimu na matumizi yake ambayo yanatawala maisha yetu ya kila siku.

Hata hivyo, kwa mwaka huu wa 2019, tutaanza na mwandishi bora wa habari zilizochapishwa katika magazeti yakiwemo matoleo ya mtadaoni (online version) pamoja na habari zilizochapishwa katika tovuti za habari (web blogs).

Kila mshiriki anatakiwa kuwasilisha nakala ya stori/makala yake (cutting) ikioneshaa gazeti na tarehe iliyochapishwa. Aidha, anatakiwa kuleta 'soft copy' ya stori/makala hiyo. Kwa stori au makala iliyochapishwa katika nakala ya mtadaoni ya gazeti (online version), au katika web blog, anatakiwa kutuma link ya stori kwenye Mtandao au web blog na makala halisi ikiwa kwenye 'soft copy'. Stori au makala zinatakiwa ziwe katika moja ya lugha rasmi zinazotumika nchini yaani Kiswahili au Kingereza. Aidha, mshiriki atajaza fomu maalum na kuirejesha ikiambatana na stori au makala yake.

Stori au Makala zitakazowasilishwa ziwe zimechapishwa kati ya Januari, 2017 hadi mwisho wa tarehe ya kufunga shindano ambayo ni tarehe 22 Novemba, 2019 saa 10:00 jioni. Washiriki wanatakiwa kutuma stori/makala zao kupitia emails zifuatazo:

sg@nbs.go.tz na nakala kwa joel.weja@nbs.go.tz, said.ameir@nbs.go.tz na mateew@gmail.com.

**FOMU YA USAJILI KUSHIRIKI SHINDANO LA MWANDISHI BORA WA
HABARI ZA KITAKWIMU**

Jina Kamili: _____

Taasisi/Chombo cha Habari: _____

S.L P: _____

Simu ya Ofisi: _____

Baruapepe ya Ofisi: _____

Jina la Mhariri/Mkuu wa Chumba cha Habari: _____

Anuani yako Binafsi: _____

Mahala unapoishi: _____

Mtaa: _____

Wilaya: _____

Mkoa: _____

Simu Binafsi: _____

Baruapepe Binafsi: _____

Kichwa cha Habari ya Stori/Makala yako: _____

Chombo cha Habari kilichochapisha stori/Makala yako: _____

Toleo na Tarehe iliyochapishwa: _____